# SERA YA USIRI

**Tarehe ya Mwisho wa Marekebisho:** 20.06.2025

Karibu SchoolMtandao, programu ya kuendesha shughuli za skuli kama vile usajili wa wanafunzi, madarasa na malipo ya ada. Tunathamini faragha ya watumiaji wetu na tumejizatiti kulinda taarifa zao binafsi. Sera hii ya usiri inaeleza jinsi tunavyokusanya, kutumia, kuhifadhi na kulinda taarifa zako.

## 1. Taarifa Tunazokusanya

Tunapokusanya aina mbalimbali za taarifa ili kuboresha huduma zetu. Taarifa hizi zinaweza kujumuisha:

- Taarifa za Skuli:
- Taarifa za Mwanafunzi
- Taarifa za kielektroniki

## 2. Jinsi Tunavyotumia Taarifa

Taarifa unazotupatia zinatumika kwa madhumuni yafuatayo:

- Kuwezesha utendaji wa mfumo wa SchoolMtandao
- Kuunda akaunti za watumiaji (wamiliki, wahasibu, wazazi)
- Kuwasiliana na watumiaji kuhusu masuala ya skuli
- Kuboresha huduma na vipengele vya programu
- Kuhifadhi kumbukumbu salama za shule

## 3. Ushirikishaji wa Taarifa

Hatutauza, kukodisha au kushirikisha taarifa zako binafsi na watu au mashirika ya nje bila idhini yako, isipokuwa:

- Pale inapohitajika kwa mujibu wa sheria
- Kwa taasisi ya serikali pale inapohitajika kwa malengo ya kisheria au kielimu

## 4. Hifadhi ya Taarifa

Taarifa zako zitahifadhiwa kwa usalama kwa kutumia mbinu za kiusalama za kisasa kama vile:

Swahili Technologies

- Usimbaji wa data (data encryption)
- Ulinzi wa nenosiri
- Ufikiaji kwa ruhusa maalum tu

## 5. Haki za Mtumiaji

Una haki ya:

- Kutazama taarifa zako binafsi
- Kufanya marekebisho ya taarifa zisizo sahihi
- Kuomba kufutwa kwa akaunti yako au taarifa zako (isipokuwa pale inapohitajika kwa rekodi za skuli)

## 6. Watoto na Faragha

Tunajua umuhimu wa kulinda taarifa za watoto. Kwa hivyo, taarifa za wanafunzi zitakusanywa tu kwa idhini na kwa mujibu wa masharti ya shule.

## 7. Mabadiliko ya Sera

Tunaweza kufanya marekebisho ya sera hii kadri inavyohitajika. Mabadiliko yote yatachapishwa kupitia mfumo na tarehe ya mwisho ya mabadiliko itaoneshwa juu ya ukurasa huu.

---

## 8. Mawasiliano

Kama una maswali au maoni kuhusu sera hii ya usiri, tafadhali wasiliana nasi kupitia:

**Barua pepe:** info@schoolmtandao.co.tz

**Simu**: 255777118463
**Tovuti**: www.schoolmtandao.co.tz

Swahili Technologies